



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Simu namba: 027-2790008  
Fax Namba: 027-2757294  
Barua pepe: [ded@rombodc.go.tz](mailto:ded@rombodc.go.tz)  
Unapojibu tafadhali taja:

MKURUGENZI MTENDAJI,  
328 BARABARA YA SABASABA,  
S.L.P 52,  
25782 MKUU-ROMBO.

Kumbu. Na. HWR/C.6019/28

16/07/2024

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI AJIRA YA MKATABA.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo anawatangazia Watanzania wote wenye sifa kuomba nafasi za Ajira ya Mkataba kwa kipindi cha miezi mitatu (03) kama ifuatavyo:

### **1.0 KUKUSANYA USHURU/MAPATO YA HALMASHAURI (NAFASI 43)**

#### **1.1 MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kukusanya mapato ya Halmashauri katika kituo atakachopangiwa.
- ii. Kutunza kumbukumbu za hesabu.
- iii. Kutunza vizuri vitendea kazi atakavyokabidhiwa ikiwemo mashine ya kukusanyia mapato (POS).
- iv. Kutoa na kuwasilisha taarifa ya makusanyo ya kila siku ya Halmashauri kwa msimamizi wake.
- v. Kuwasilisha fedha za makusanyo Benki katika Akaunti ya Halmashauri kwa muda atakaopangiwa na Mwajiri.
- vi. Kufanya kazi nyingine zote atakazopangiwa na Mwajiri/Msimamizi wa kituo cha kazi.

#### **1.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Awe amehitimu Elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
- ii. Awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote atayopangiwa na Mwajiri.
- iii. Awe na akili timamu, muaminifu na muadilifu.
- iv. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- v. Awe na uwezo wa kutumia simu janja/POS.
- vi. Waombaji wenye Elimu ya Astashahada na kuendelea katika fani ya Biashara/Uhasibu, ujuzi wa kutumia computer, wenye fani ya udereva na wenye kumiliki pikipiki binafsi watapewa kipaumbele zaidi.

#### **1.3 MSHAHARA**

Mshahara kwa mwezi ni asilimia kumi (10%) ya mapato utakayokusanya katika kituo cha kazi ulichopangiwa.

## 2.0 WAHUDUMU WA KUFANYA USAFI (NAFASI 03)

### 2.1. MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kufanya usafi wa ofisi na mazingira ya nje na ndani ya eneo la kazi utakalopangiwa ikiwa ni pamoja na kufagia, kudeki, kufuta vumbi, kufyeka majani, kupalilia bustani za maua, kumwagilia maji bustani, kupanda maua au miti na kusafisha vyoo.
- ii. Kufungua milango na madirisha ya ofisi/ukumbi wakati wa asubuhi na kufunga jioni baada ya saa za kazi.
- iii. Kutunza vifaa na mali nyingine zote atakazokabidhiwa na Mwajiri.

### 2.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe amehitimu Elimu ya kidato cha nne na kuendelea.
- ii. Awe na akili timamu, muaminifu na muadilifu.
- iii. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- iv. Waombaji wenye ujuzi katika fani ya usafi na utunzaji wa bustani watapewa kipaumbele.

### 2.3 MALIPO YA POSHO

Malipo ya posho ya shilingi elfu nane (8,000/=) yatatolewa kwa kila siku utayofanya kazi.

### 3.0 MASHARITI YA JUMLA:

- I. Mwombaji aambatishe nakala ya vyeti vya (Taaluma). Cheti cha kidato cha nne/sita, cheti cha kuzaliwa na picha mbili za "passport size" za hivi karibuni na ziandikwe majina kwa nyuma.
- II. Mwombaji asiwe amewahi kuhukumiwa na mamlaka yoyote kwa kosa la jinai au makosa mengine ya kukosa uaminifu/uadilifu.
- III. Mwombaji awe na wadhamini wawili (02) watakaotambulishwa na serikali ya mtaa/kijiji.
- IV. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina sahihi.
- V. Mwombaji awe na kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kitambulisho cha mpiga kura
- VI. Maombi yote yawasilishwe masijala ya Mkurugenzi Mtendaji au kupitia barua pepe [ded@rombodc.go.tz](mailto:ded@rombodc.go.tz).
- VII. Watumishi wote wenye mikataba ya Ajira ya muda ya kukusanya ushuru/kufanya usafi katika Halmashauri ya Wilaya Rombo kwa sasa wanatakiwa kutuma maombi yao ya kazi upya.
- VIII. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 30/07/2024 saa 9:30 Alasiri.

**Tangazo hili linafuta tangazo la tarehe 09/07/2024 lenye Kumb.  
Na.HWR/S.20/28/13.**



Godwin J. Chacha

**MKURUGENZI MTENDAJI (HWA)  
MKURUGENZI MTEJWA  
ROMBO  
HALMASHAURI YA WILAYA  
ROMBO**